**JESMA 002**

# JARIBIO LA PILI K.C.P.E
# DARASA LA NANE 2020

**KISWAHILI
SEHEMU YA
KWANZA:
LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

    **Mfano**

    **Katika kijitabu cha maswali:**

    **11.** Chagua jibu lenye nomino zilizo katika ngeli ya I - I pekee.
    A. kahawa, fedha;
    B. chumvi, chupa
    C. sukari, mvua
    D. mali, chai

    Jibu sahihi ni C

    | | | | | |
    |---|---|---|---|---|
    | 1 [A] [B] [C] [D] | 11 [A] [B] ■ [D] | 21 [A] [B] [C] [D] | 31 [A] [B] [C] [D] | 41 [A] [B] [C] [D] |

    Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.
11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi* **1** *mpaka* **15.** *Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.*

__**1**__ . Tabia ya mtoto __**2**__ na walio na mamlaka __**3**__ yake. Hii __**4**__ sababu ya kuwaona watoto wengi __**5**__ matendo ya watu wazima kama vile __**6**__ kupakata vitoto bandia, kupika, kuendesha vigari vyao na kazi kama vile ualimu na udakatari. __**7**__ mzazi ana __**8**__ isiyonyooka kama vile kuvuta sigara na lugha ya matusi, basi __**9**__ kumwona mtoto wake akizifuata nyayo zizo hizo.

**1.** A. Ukibebwa usilevye levye miguu B. Mwana akibebwa hutazama kisogo cha nina C. Tabia ni ngozi ya mwili D. Baniani mbaya kiatu chake dawa

**2.** A. huathiriwa B. huathiria C. hurithika D. huathirishia

**3.** A. dhidi B. mbele C. baina D. juu

**4.** A. ndio B. ndizo C. ndiyo D. ndilo

**5.** A. wakiwaiga B. wakiziiga C. wakiyaiga D. wakijiiga

**6.** A. ; B. : C. , D. ...

**7.** A. Ikiwa B. Ingawa C. Lau D. Ilhali

**8.** A. matendo B. nyendo C. maandili D. mienendo

**9.** A. itashangaza B. isingeshangaza C. haitashangaza D. ingeshangaza

"__**10**__ nitakusaidia kuimarika," akasema Mwalimu Pendo. "Maadamu umeonyesha __**11**__, yaani hamu ya __**12**__ matokea yako katika Kiswahili, sitakuhini msaada huo." Maneno yako yalinitia matumaini mapya. Darasa __**13**__ __**14**__ na mwamko wangu mpya. Sikuwa yule Patu aliyezoea __**15**__ darasani bali nilivalia joho jipya la bidii na nidhamu wakati wote.

**10.** A. la B. shabash C. ashakum D. hewala

**11.** A. ari B. hari C. shaka D. fedheha

**12.** A. kuiboresha B. kuyaboresha C. kuliboresha D. kuziboresha

**13.** A. mzima B. nzima C. wazima D. zima

**14.** A. walishangazwa B. lilishangazwa C. ilishangazwa D. mlishangazwa

**15.** A. kupiga mbiu B. kutia nanga C. kulaza damu D. kupiga debe

*Kuanzia nambari 16 mpaka 30, chagua jawabu lifaalo zaidi.*

**16.** Maelezo yapi SI sahihi?
A. Paa ni kuchukua makaa yenya moto.
B. Paa ni kuondoa magamba ya samaki.
C. Paa ni kumkabidhi mtu kitu.
D. Paa ni kuelea kwenye anga.

**17.** Chagua umoja wa sentensi ifuatayo:
Nyaadhi hizo zilitolewa na makungwi stadi.
A. Nyaadhi hiyo ilitolewa na kungwi stadi.
B. Waadhi huo ulitolewa na kungwi stadi.
C. Waadhi hiyo ilitolewa na kungwi stadi.
D. Nyaadhi hiyo ilitolewa na makungwi stadi.

**18.** Andika usemi wa taarifa wa sentensi ifuatayo:
"Shamba hili lina mimea iliyostawi vizuri," akasema.
A. Anasema kwamba shamba hili lina mimea iliyonawiri vizuri.
B. Angesema kwamba shamba hili lilikuwa na mimea iliyonawiri vizuri.
C. Alisema kwamba, shamba hilo lilikuwa na mimea iliyonawiri vizuri.
D. Alisema kwamba shamba hilo huwa na mimea iliyonawiri vizuri.

**19.** Seremala akitaka kutoboa mbao hutumia chombo kipi?
A. msasa
B. randa
C. timazi
D. kekee

**20.** Tambua sentensi yenye __ni__ kuonyesha nafsi.
A. Aliponitembelea hatukuonana.
B. Watalii wamejilaza ufuoni.
C. Usidhani kuwa yeye ni mpole.
D. Mgonjwa alikuwa taabani tulipofika.

**21.** Andika kinyume cha sentensi hii
Ajuza ameanika nguo.
A. Ajuza amaeanua nguo.
B. Shaibu hajaanika nguo.
C. Buda ameanua nguo.
D. Kijana hajaanika nguo.

**22.** Nimino zipi huorodheshwa katika ngeli ya I - I pekee?
A. Mamlaka, mbua
B. Sukari, asali
C. Mali, fedha
D. Chupa, baridi

**23.** Nge ni kwa kisuse kama ilivyo **nzige** kwa
A. kimatu
B. kiyoyo
C. kiwavi
D. king'onyo

**24.** Unda kivumishi kutokana na kitenzi **cheka**.
A. chekesha
B. mcheshi
C. cheshi
D. kicheko

**25.** Maelezo yapi ni sahihi?
A. Utenzi ni shairi la majibizano.
B. Mizani ni silabi za katikati ya mishororo.
C. Ngonjera ni shairi lenye beti nyingi.
D. Arudhi ni kanuni zinazoongoza utunzi wa mashairi.

**26.** Chagua **kielezi** katika sentensi ifuatayo.
Vipindi vya vibonzo aghalabu hufurahisha watoto wengi.
A. wengi
B. hufurahisha
C. aghalabu
D. vya vibonzo.

**27.** Tumia kiunganishi kifaacho kuunganisha sentensi hizi.
Bikizee hakuwa na furaha. Bikizee alikua na huzuni.
A. Bikizee hakuwa na furaha wala huzuni.
B. Bikizee hakuwa na furaha bali huzuni.
C. Bikizee hakua na furaha angalau huzuni.
D. Bikizee hakuwa na furaha ingawa huzuni.

**28.** Kitenzi kipi hakionyeshi kauli sahihi ya kutendesha?

A. nasa
B. Washa
C. ogofya
D. kimbisha

**29.** Ni kauli ipi inayoonyesha **sitiari**?

A. Nimechoka mithili ya punda wa dobi.
B. Mwanaisha ni chirika darasani.
C. Moyo wangu uliniambia kulikuwa na hatari.
D. Vijana wale waliangua kicheko kwa kwa kwa.

**30.** Ni orodha ipi iliyo na vivumishi pekee?

A. wale, vyote, sana, lipi
B. tele, chafu, gumu, kingine.
C. kadhaa, wenyewe, jiriwa, lo
D. ala, lakini, hicho, tamu

*Yasome makala yafuatayo kisha ujibu maswali kuanzia* **31** *mpaka* **40**

Mzee Changu alichukiza kila mwanakijiji kwa hulka yake ya kukaripia watu. Lau angejua tabia hiyo si nzuri, angeiacha mara moja. Alilifahamu hilo kwa uchungu chungu nzima alipoangukiwa na balaa.

Siku hiyo ilikuwa ni Jumapili asubuhi waumini wakienda kumtukuza Jalali. Njia ya kuelekea kanisani ilipasua shamba la Mzee Changu. Wakati huo alikuwa amerauka alfajiri na mapema kupalilia mihogo yake. Kundi la kwanza la takriban watu kumi lilipita huku likiimba nyimbo za sifa. Kumbe changu hakufurahia.

"Hebu fanyeni heshima! Watu wengine wamelala, kelele za nini?" Aliwaendea huku mdomo ukimcheza. Punde si punde kundi jingine kubwa likapitia njia iyo hiyo. Nao vile vile walikuwa wakipaaza sauti zao kwa nyimbo kem kem. Hilo **lilimgusa mshipa** Changu. Alifululiza hadi katikati ya nji na kutanua lile jifua lake pana mithili ya ngao. "Haya rudini mlikotoka. Njia hii naifunga leo hadi siku ya hukumu", Alisema huku jembe li mkononi akiwatishia waumini warudi nyuma.

Waumini walilalamika lakini ilibidi wasalimu amri. Waligeuza njia. Mzee Changu alikusanya miti ya miiba na magogo na kuifunga njia. Waja waliozoea kupasulia weu hapo walishangazwa na kitendo hicho lakini walichelea kumkabili changu. Ni nani angethubutu kuukabili mtambo wenye kumimina vipande vya matusi!

Mzee Changu alipokuwa akiyachoma majani makavu, nyumba yake ilirukiwa na cheche za moto. Paa likaanza kuchomeka. Wakati huo waumini walikuwa wakirejea mastakimuni baada ya ibada.

"Njooni jamani! Njooni watu wa Mungu mnipe mkono!" Changu aliita na kuomba msaada. Alisahau kwamba ilikuwa vigumu kuingia katika boma lake lililozungushiwa miti ya miba. Nafasi iliyokuwepo ni ile njia aliyoifunga kwa magogo na miba mikali.

"Basi iondeo hiyo miiba na magogo ili tuje kuuzima moto," mtu mmoja alimwambia. Mzee Changu alifanya hivyo kwa dhiki kubwa, huku paa la makuti likiliwa na moto. Alipolitimisha kuondoa miiba, paa lilikuwa limemalizika. Watu waliingia na kuuwahi moto kabla haujaleta uharibifu mkubwa zaidi.

Baada ya kuuzima moto, mhubiri aliyekuwepo akamwambia, "Rudi uizibe njia yako maana tunatoka." Mzee Changu alitahayari na kusema, "Tangu leo njia iko wazi, piteni na muimbe mtakavyo."

**31.** Chagua jawabu lililo sahihi. Mzee Changu
A. alipenda kuwagombeza watu.
B. alizoea kupigana na watu.
C. alichukizwa na hulka ya wanakijiji
D. hakuwahi kujua anawaudhi watu.

**32.** Njia ya kuelekea kanisani ilipitia
A. karibu na nyumba ya Changu.
B. kando ya shamba la Changu.
C. katikati ya mihogo ya Changu
D. ndani ya shamba la Changu.

**33.** Ni kweli kusema kuwa,
A. waumini walipuuza maslahi ya wengine.
B. Changu hakupenda watu waharibiwe usingizi.
C. Mzee alitaka tu kuanzisha mgogoro.
D. Changu hakufurahia kuingiliwa kwenye shughuli zake.

**34.** Maneno **lilimgusa mshipa** yana maana kuwa
A. lilimshangaza
B. lilimkirihi
C. lilimhuzunisha
D. lilimfurahisha.

**35.** Mzee Changu anaweza kutajwa kuwa,
A. gofu la mtu
B. tambo la mtu
C. fremu ya mtu
D. kifyefye cha mtu

**36.** Tendo la kuziba njia kwa miba na magogo linaonyesha kuwa Changu ni mtu mwenye sifa ya
A. inda
B. uchochezi
C. ukatili
D. ulafi

**37.** Kwa nini watu walisalimu amri mbele ya Changu
A. walijua kuwa huenda akawashtaki.
B. walikuwa waumini wasiopenda ugomvi.
C. walitishiwa na aila ya Changu kwa jembe.
D. walichelea kubwagiwa matusi.

**38.** Kitendo cha kuchomeka kwa nyumba ya Changu;
A. kilikuwa ni ajali ya kawaida tu.
B. kilitokana na hasira ya waumini.
C. ni ulipizaji kisasi wa waliodhulumiwa.
D. Alikifanya makusudi ili kuwavuta watu.

**39.** Mhubiri alipomwita Mzee Changu aizibe njia tena,
A. alijua kuwa watu hawaihitaji njia hiyo.
B. alinuia kumdhihaki mzee Changu.
C. alifahamu kuwa Changu angeifunga tu.
D. alitaka nyumba ile iteketee kabisa.

**40.** Kichwa kifaacho **zaidi** kwa taarifa hii ni
A. pwagu hupata pwaguzi.
B. Bahati ni chudi
C. Mtu ni watu
D. Usiwatukane wakunga na uzazi ungalipo.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali kuanzia* **41** *mpaka* **50**

Usalama katika jamii nikigezo muhimu katika ukuaji wa uchumi wa taifa. Taifa lililo salama huhakikisha mazingira bora ya kibiashara na husababisha mvuto kwa wawekezaji wa nchi wa wale wa kigeni. Kwa upande mwingine, jamii isiyo na usalama hukosa umoja na mishikamano, jambo linalosababisha kudorora kwa uchumi.

Katika nchi yetu usalama ni tatizo sugu. Barabara zetu si salama. Kila uchao visa vya vifo kutokana na ajali za barabarani huripotiwa. Baadhi ya vifo husababishwa na barabara mbovu , ufisadi wa maafisa wa trafiki, magari mobovu na udhaifu wa madereva hasa wa magari ya usafiri wa umma. Zaidi ya vifo, ajali hizi husababisha uyatima na uharibifu wa mali na miundo msingi. Utekaji nyara wa wasafiri barabarani ni tatizo jingine. Baadhi ya mateka huwa ni watalii, jambo hili husababisha kupungua kwa watalii wanaozuru taifa letu.

Aidha ukosefu wa usalama huathiri biashara. Wafanyabiashara rejareja hawana uhuru wa kufanya kazi zao usiku wakihofia uvamizi wa majambazi. Wawekezaji pia hukosa imani na hali ya usalama na huishia kuwekeza katika mataifa wanayohisi kuwa ni salama zaidi.

Visa vya ubakaji na ulawiti wa watoto vimezidi katika maeneo mbalimbali. Jambo hili linawafanya wavyele na wanawake kwa jumla kuwa na jakamoyo wanapoendelea na shughuli zao za kila uchao. Kuwepo kwa makundi haramu ya kuhalifu ni ithibati ya jamii inayoishi katika hofu. Makundi haya huvamia wananchi usiku na kuwachinja kama mbuzi. Kero jingine ni utamaduni wa wizi wa mifugo unaendelezwa na baadhi ya jamii. Katika wizi huu, maisha hupotezwa na mali kuharibiwa.

Swali kuu ni je, nini kitovu cha ukosefu huu wa usalama? Kwa mujibu wa ripoti za wakuu wa usalama, hali hii huchagiwa zaidi na ukosefu wa ajira hususan kwa vijana, jambo linalowafanya kutumiwa kuzua vurugu au wakajiunga na makundi haramu. Kusambaratika kwa familia na ulegevu wa wavyele katika kutekeleza majukumu yao pia ni sababu nyinginezo. Isitoshe, utepetevu wa walinda usalama, uchechefu wa vifaa bora na ukosefu wa ushirikiano wa raia huchangia hali hii kwa kiasi kikubwa.

Ni muhimu kuunga mkono kauli ya rais kuwa **usalama huanza na mini na wewe**. Kila mwanajamii anastahili kuripoti wahalifu kwa walinda usalama popote awaonapo. Serikali nayo ihakikishe kuna idadi tosha ya walinda usalama nchini. Aidha ni jukumu la serikali kuhakikisha kwamba kuna vifaa vya kutosha kutumiwa na vyombo vya dola nchini.

**41.** Kulingana na aya ya kwanza,
A. hali ya utulivu huchangia ustawi nchini.
B. usalama katika nchi hutegemea mazingira yalivyo.
C. usalama hutegemea pakubwa uchumi wa taifa.
D. mataifa yaliyostawi hukabiliwa na utovu wa usalama.

**42.** **SI** kweli kusema kuwa,
A. utovu wa usalama unaweza kuvuruga utangamano.
B. kusiko na usalama kuna uhaba wa wawekezaji.
C. Wenyeji pekee ndio kuwekeza kule kusiko na usalama.
D. kukosekana kwa usalama hupunguza nafasi za kujiendeleza.

**43.** Visa vya ajali za barabarani
A. Vimeadimika kama wali wa daku
B. Vimeripotiwa mara kwa mara.
C. Vimekuwa vikishuhudiwa bila kutajwa
D. Vimezidi kuliko maovu mengine yote.

**44.** Yote haya yametajwa kuwa huchangia ajali za barabarani **ILA**
A. watu kuzunguka mbuyu.
B. barabara kukosa kukarabatiwa.
C. kutowajibika kwa madereva.
D. udhaifu wa madereva kimaumbile.

**45.** Kwa nini watalii wamepungua nchini?
A. ajali za barabarani zimewakosesha usalama.
B. uchumi wa nchi unaendelea kudorora.
C. vivutio vingi vya kitalii vimeharibiwa.
D. visa vya utekajinyara vimewafanya kuhofu.

**46.** Biashara huathiriwa vipi na ukosefu wa usalama?
A. wawekezaji hugura na kuwekeza kukiko na utulivu.
B. wengi hukata tamaa na kuacha biashara kabisa.
C. wafanya biashara wengi huingilia vitendo vya uhalifu.
D. biashara nyingi hunawiri vyema kusiko na utulivu.

**47.** Visa vya ubakaji na ulawiti vimefanya wazazi,
A. kushtuka sana.
B. kuwa na wasiwasi.
C. kuwatekeleza watoto.
D. kuacha shughuli zao.

**48.** Utamaduni usiofaa kulingana na mwandishi hapa ni,
A. kujiunga na makundi haramu.
B. wavyele kuwatelekeza watoto.
C. visa vya wizi wa mifugo.
D. kudhulumiwa kwa watoto kimapenzi.

**49.** Maoni ya mwandishi wa makala haya ni kuwa,
A. wanaokosa njia za kujiendeleza huweza kuandama hulka zisizofaa.
B. umaskini wa wazazi umewafanya kupuuza malezo yanayofaa.
C. machafuko ya kisiasa hufanya vijana wajiunge na makundi yasiyoidhinishwa.
D. kutojua majukumu yao kumewafanya wazazi wengi kutowajibika.

**50.** **'...usalama unaanza na mimi na wewe...'** ndiko kusema,
A. ukosefu wa usalama hutokana na walio karibu na mtu.
B. ukosefu wa usalama kuchangia na watu kutojuana
C. udumishaji wa usalama ni kujumu la serikali yoyote ile.
D. udumishaji wa usalama unahitaji machango wa kila mmoja.